

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI

Simu: +255-26-2323201-7
Nukushi: +255-26-2323208
Barua pepe: nje@nje.go.tz
Tovuti: www.foreign.go.tz



Mji wa Serikali,
Mtumba,
S.L.P 2933,
40466 DODOMA.

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. QA 298/485/01

20 Aprili 2022

Waheshimiwa Mabalazi,

BALOZI ZOTE ZA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA.

YAH: HUDUMA ZA BENKI YA CRDB ZILIZOBORESHWA KWA AJILI YA DIASPORA

Tafadhali husika na somo tajwa hapo juu.

2. Wizara imepokea barua kutoka Benki ya CRDB PLC iliyowasilisha taarifa kuhusu huduma mbalimbali za benki hiyo zilizoboreshwa kwa ajili ya mahitaji ya Diaspora.
3. Huduma hizo zitakuwa zinashughulikiwa na Kitengo Maalum kwa ajili ya Diaspora (*Diaspora Banking Unit*) kilichopo chini ya benki hiyo na Mameneja wafuatao:

Kitengo cha Benki – Diaspora		
Namba ya simu ya mezani: +255(0)222 212926 na +255(0)222 212927		
Barua pepe: tanzanite@crdbbank.co.tz		
Bw. Gibson Mlaseko	Meneja Mwandamizi	Gibson.mlaseko@crdbbank.co.tz
Bw. Joseph Haule	Meneja Mahusiano Mwandamizi	Joseph.haule@crdbbank.co.tz
Bi. Mercy Nkini Bi. Hellen Steven Bw. Godson Masha	Mameneja Mahusiano	tanzanite@crdbbank.co.tz

4. Huduma zinazotolewa na benki ya CRDB kwa ajili ya Diaspora ni:

- (i) **Akaunti maalum ya akiba ya Tanzanite:** Diaspora anaweza kupata huduma ya mikopo ya ununuzi na ujenzi wa nyumba, huduma ya kutuma/kupokea fedha, kupata ushauri wa uwekezaji wa hisa zinazouzwa na soko la hisa Dar es Salaam (DSE), na huduma za bima ya KAVA. Akaunti

hiyo pia inatoa huduma za kibenki kwa njia ya mtandao (internet banking) na kwa njia ya simu (sim-banking);

- (ii) **Mkopo wa ununuzi na ujenzi wa nyumba za makazi (mortgage financing):** Riba ya mkopo ni nafuu kwa asilimia kumi na tatu (13%) kwa mwaka;
- (iii) **Bima maalum ya KAVA Assurance:** bima hii ni maalum kwa mhusika wa akaunti na mwenza wake; inaweza kutumika pale msiba unapotokea nje ya nchi ambapo benki ya CRDB itatoa mkono wa pole wa TZS 5,000,000/- na kuchangia gharama za kusafirisha mwili wa marehemu Tanzania hadi kufikia kiasi cha TZS 15,000,000/- pamoja na tiketi ya ndege katika daraja la uchumi kwa msindikizaji wa mwili wa marehemu;
- (iv) **Huduma za kutuma na kupokea fedha nyumbani:** Diaspora wanaweza kutuma fedha zao kupitia akaunti ya benki ya CRDB kwa kutumia makampuni makubwa ambayo benki hiyo hushirikiana nayo (Western Union, WorldRemit na Ria). Diaspora pia anaweza kufanya miamala ya fedha kwa urahisi kutoka benki moja kwenda nyingine (kupitia akaunti yake ya CRDB).

5. Wizara inaomba Diaspora na Watumishi kwenye Balozi zote wahamasishwe kuchangamkia fursa hizo zinazotolewa na Benki ya CRDB kwa ajili ya huduma binafsi na kuendelea kuchangia maendeleo nchini.

Wizara inatoa shukrani za dhati kwa ushirikiano wenu.



Tagie Daisy Mwakawago
Kny: KATIBU MKUU

Viamb.../